**OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE**


**SHULE YA SEKONDARI KWEMDIMU,**
**S.L.P 55**
**MOMBO**
**12.12.2020**
**SIMU: 0657936514 MKUU WA SHULE**
**0654505032 MAKAMU MKUU WA SHULE**


**KUMB. Na. KSS/FK/2021**
JINA LA MWANAFUNZI ________________________________
S.L.P __________________________________________________

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021 SHULE YA SEKONDARI KWEMDIMU ILIYOKO HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE MKOA WA TANGA.**

## 0.1 UTANGULIZI.

Ninafuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa mwaka 2021 katika shule ya Sekondari Kwemdimu.

Muhula wa kuanza masomo unaanza Tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shule kuanzia Tarehe 11.01.2021 na mwisho wa kuripoti ni Tarehe 24.01.2021. Hata hivyo unatakiwa kuripoti ndani ya muda uliopangwa ili kuepuka kupitwa na masomo kwani masomo yataanza mara tu baada ya kufunguliwa shule. Endapo hutaripoti kwa muda uliowekwa unaweza kupoteza nafasi yako ingawaje utachukuliwa hatua stahiki.

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 Sare za shule pamoja na nguo za michezo

**WAVULANA**

- Suruali 2 rangi ya BLUE BAHARI (kitambaa grade one) na zifuate mshono/mtindo wa shule
  N.B Upana wa suruali usipungue nchi 18 Suruali ya kubana haitakubaliwa hivyo maelekezo yazingatiwe usije kuingia hasara ya kurudia kushona suruali kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa.
- Shati 2 nyeupe mikono mifupi tetroni
- Soksi ndefu nyeusi pea 2
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba jozi 2.
- Tai mbiliza kufanana na suruali.
- Sweta rangi ya **BLUE BAHARI**.
- VIFAA VYA MICHEZO:
  -Bukta rangi ya Kijani/nyekundu
  -Raba nyeupe
  -Sox ndefu za kijani/nyekundu

**NB:** Vitu vyote mwanafunzi aje navyo siku ya kuripoti shule vikaguliwe fundi atakuwepo kuhakiki vipimo ikiwa vimezingatiwa ama vinginevyo.

**WASICHANA**

- Sketi 2 rangi ya **BLUE BAHARI** kitambaa kizito Grade one kisichoonyesha, na sketi inapaswa kuwa ndefu isipungue sentimeta 15 toka kwenye unyayo urefu, mshono rinda boksi
- Neck tai mbili za kufanana na sketi
- Shati 2 nyeupe za tetroni mikono mifupi bila urembo
- Viatu vya ngozi vya kamba jozi 2 kisigino kifupi
- Soksi ndefu nyeupe pea 2 bila urembo

- Sweta rangi ya **BLUE BAHARI** NB: Vitu vyote mwanafunzi alivyoagizwa aje navyo siku ya kuripoti shule ili vikaguliwe na fundi atakuwepo ili kuhakiki vipimo ikiwa viko sawa ama vinginevyo.

**NB: HIJABU.** Hijab kwa waislamu ambao wanapenda. Sio lazima Rangi ifanane na sare ya shule.

VIFAA VYA MICHEZO

-T-Shert ya kijani /nyekundu

- traki suit ya kijani /nyekundu

-Raba nyeupe. NB: Aje navyo siku ya kuripoti vitakaguliwa.

**2.2. VIFAA VYA KUJIFUNZIA**

- Daftari kubwa zisizopungua 12, kalamu, na mathematical set.
- Begi la kubebea madaftari na vitabu .
- Oxford Dictionary kwaajili ya kujifunzia

**VIFAA VINGINE NJOO NA**.

- Jembe 1
- Kwanja 1
- Fagio 1
- Ndoo ndogo 1

3.0 . Kutokana na sheria ya Elimu ya mwaka 1978, pamoja na sheria zingine makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa na kusimamishwa shule

(a) Wizi
(b) Uasherati na ushoga
(c) Ubakaji
(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi kubeli n.k
(e) Kupigana au kupiga
(f) Kudharau bendera ya Taifa
(g) Kuwa mjamzito au kupata mimba
(h) Kuoa au kuolewa
(i) Kugoma, kuchochea na kuongeza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule
(j) Kukataa adhabu kwa makusudi
(k) Kutoa mimba
(l) Kuwa na simu ya mkononi

4.0. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi

(a) Medica Examination Form ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa hospitali ya Serikali Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
(b) Fomu ya maelezo binafsi ya kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
(c) Fomu ya mzazi kukiri kukabiliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule
(d) Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

***KARIBU SANA KATIKA SHULE HII***

______________________________

***EMANUEL LALA BAYO***

***MKUU WA SHULE.***

**SHULE YA SKEONDARI KWEMDIMU KUTWA**
**HISTORIA YA MWANAFUNZI**

**MWANAFUNZI**

Jina ____________________________________________

Tarehe ya kuzaliwa _______________________________

Dini _____________________________________________

Shule uliyotoka __________________________ Tarehe ________________ Sahihi _____________

**MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.**

Mimi ___________________________________ nimesoma na kuelewa makosa yote ambayo yatasababisha kufukuzwa shule/ kusimamishwa shule katika fomu ya kujiunga.

Naahidi kutoshiriki katika makosa haya. Endapo nitashiriki nisimamishwe/nifukuzwe shule

Jina _________________________________ Sahihi ________ Tarehe ___________

**FOMU YA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE.**

Mimi __________________________________ mzazi/mlezi wa mwanafunzi ____________________. Nakubaliana na sheria kanuni na maelezo mengine yaliyotolewa na shule katika fomu ya kujiunga. Aidha nitahakikisha anahudhuria shule kila siku kwa mujibu wa sheria.

Naahidi kwamba nisipofanya hivyo hatua za kinishamu zichukuliwe juu yangu

Jina _________________________________ Sahihi ______ Tarehe ____________

**NB. FOMU HII IWE IMEJAZWA NA DAKTARI WA HOSPITALI YA SERIKALI UTALETA SHULE SIKU YA KWANZA UNAPOKUJA KUMKABIDHI (kuripoti) MWANAO SHULENI IKIWA IMEJAZWA NA DAKTARI WA HOSPITALI YA SERIKALITAYARI.**

# OFISI YA RAIS TAMISEMI
# HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE (V).

## SHULE YA SEKONDARI KWEMDIMU

## (B). REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

**KWEMDIMU SECONDARY,**

**P.O.BOX 55,**

**MOMBO.**

**DATE 12.12.2021.**

**MEDICAL OFFICER,**

…………………………………………………………………..GOVERNMENT HOSPITAL/ H.C. (Jina la Hospitali ya serikali).

**NAME OF STUDENT:………………………………………………………………………………………………………………**

Please examine the above named student to ascertain his/her fitness for further studies.

……………………………………………………………..

**HEAD OF SCHOOL.**

**MEDICAL CERTIFICATE:**

[To be completed by the medical officer].

I have examined the above named students with regard to:

Skin ……………………………Eyes,………………………Ear………………Chest………………Eyes …………………………… Spleen ………………… Abdomen …………………… Urine ……………………………………Stool ……………………… Hemoglobin …………………… Sickle cell …………………………………………………others……………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

**And I considered.**

**1.**He/She is good health, free from infection diseases, worms, bilharzias, and fit to go to school.

**2.** He/She is now to return to school having treatment ………………………………………………………………………………

name & signature of medical officer ……………………………………………………………………………………………….

**Date:** …………………………………………………………………

**NB. <u>FOMU HII IWE IMEJAZWA NA DAKTARI WA HOSPITALI YA SERIKALI UTALETA SHULE SIKU YA KWANZA UNAPOKUJA KUMKABIDHI (kuripoti) MWANAO SHULENI IKIWA IMEJAZWA NA DAKTARI WA HOSPITALI YA SERIKALITAYARI.</u>**